



MWITO Wa KUTOA MAONI

(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (Shinyanga WSSA) (“Muombaji”) kwa ajili ya kutoa huduma za Maji na Usafi wa Mazingira katika Miji ya Tinde, Iselamagazi, Didia na Manispaa ya Shinyanga, Mkoa wa Shinyanga. EWURA inakaribisha maoni kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Muombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:-

1: Jina na Anuani:

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga,
S.L.P 298,
Shinyanga.
Tanzania.
Barua Pepe: info@shuwasa.go.tz

2: Maelezo ya Leseni:

Leseni ya kutoa huduma za Maji na Usafi wa Mazingira katika Miji ya Tinde, Iselamagazi, Didia na Manispaa ya Shinyanga

3: Chanzo cha Maji na Miundombinu

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga ina vyanzo vikuu vinne (4) vya maji ambavyo ni visima virefu vilivyopo Tinde na Didia, bwawa la Ning’wa na Maji kutoka Ziwa Victoria ambayo hununuliwa kwa jumla kutoka KASHWASA.
Uwezo wa kuzalisha maji kwa maeneo yote ni mita za ujazo 48,128 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji inajumuisha matenki ya maji 11 yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 22,837. Muombaji pia ana mtandao wa maji wenye urefu wa kilomita 620, pamoja na magati 315.

4: Umiliki



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi
S. L. P 2857, Dodoma.

Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;

Namba ya Bure 0800110030;

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>